



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU TAKWIMU ZA WAPIGA KURA NA VITUO VYA KUPIGIA KURA
VITAKAVYOTUMIKA KATIKA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2025

Arusha, 07 Oktoba, 2025

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) imepokea taarifa kutoka Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) kuhusu mabadiliko ya takwimu za idadi ya wapiga kura na vituo vya kupigia kura vitakavyotumika katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Taarifa hiyo imetolewa baada ya kukamilika rasmi kwa uchakataji wa taarifa za wapiga kura waliopo kwenye Daftari la Wapiga Kura la Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) ambapo takwimu zake ni kama ifuatavyo: -

- i. idadi ya wapiga kura walioandikishwa ni 717,557; na
- ii. idadi ya vituo vya kupigia kura ni 1,752.

Kutokana na mabadiliko ya takwimu za wapiga kura na idadi ya vituo vya kupigia kura yaliyowasilishwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar, idadi ya wapiga kura na vituo vya kupigia kura vilizotangazwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi tarehe 26 Julai, 2025 imebadilika kama ifuatavyo: -

1. Idadi ya wapiga kura

- i. Jumla ya wapiga kura waliopo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 ni 37,647,235 badala ya 37,655,559 iliyotangazwa awali.

Idadi hiyo ya wapiga kura 37,647,235 ni sawa na ongezeko la asilimia 26.53 kutoka idadi ya wapiga kura 29,754,699 waliokuwa kwenye Daftari la Wapiga Kura mwaka 2020;

- ii. Kati ya wapiga kura 37,647,235, wapiga kura 36,650,932 wapo Tanzania Bara na Wapiga Kura 996,303 wapo Tanzania Zanzibar; na



- iii. Kati ya idadi ya wapiga kura 37,647,235, wanawake ni 18,950,801 sawa na asilimia 50.34 na wanaume ni 18,696,439 sawa na asilimia 49.66.

2. Idadi ya Vituo vya Kupigia Kura Mwaka 2025

- i. jumla ya vituo vya kupigia kura vitakavyotumika kwenye Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 itakuwa ni 99,895 badala ya 99,911 iliyotangazwa awali baada ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kufanya marekebisho ya vituo vya kupigia; na
- ii. mgawanyo wa vituo hivyo kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ni kama ifuatavyo: -
 - (a) idadi ya vituo kwa Tanzania Bara vitakuwa ni 97,348;
 - (b) idadi ya vituo kwa Tanzania Zanzibar itakuwa ni 2,547.

Idadi hiyo ya vituo 99,895 ni sawa na ongezeko la asilimia 22.47 ya vituo vya kupigia kura 81,567 vilivyotumika katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, uandikishaji wa wapiga kura kwa upande wa Tanzania Zanzibar kwa ajili ya uchaguzi wa Rais na Wabunge, unazingatia sheria inayohusu uandikishaji wa wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar pamoja na mabadiliko yatakayofaa. Hivyo, Daftari la Wapiga Kura la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar litakuwa ni sehemu ya Daftari la Wapiga Kura la Tume ya Huru ya Taifa ya Uchaguzi kwa ajili ya uchaguzi wa Rais na Wabunge upande wa Tanzania Zanzibar.

Tume itavipatia vyama vya siasa vinavyoshiriki Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, orodha ya vituo vya kupigia kura vya Tume ya Huru ya Taifa ya Uchaguzi vitakavyotumika kwenye uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2025.

Imetolewa na:


Kallima, R. K.

MKURUGENZI WA UCHAGUZI



“KURA YAKO HAKI YAKO JITOKEZE KUPIGA KURA”